# LEARNING BY EAR

## "MGENI KIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA"

**KIPINDI CHA TATU: "ISHARA NA MATIBABU"**

**SCRIPT: CHRISPIN MWAKIDEU**
**EDITOR: ANDREA SCHMIDT**
**ASSISTANT EDITOR: Katrin Ogunsade**
**Health Expert: Dr. Heidrun Hübner**

**List of characters for episode 3:**

- MASIKA (40)
- BETTINA (34)
- KAREMBO(14)
- ZAWADI (BABY, no actor needed))
- H/TEACHER (38)
- MAMA DAVID (43)
- DAVID (14)
- NARRATOR/Intro-Outro

**INTRO/NARRATOR (same voice):**

Hujambo msikilizaji na karibuni tena katika sehemu ya tatu ya kipindi cha Noa Bongo jenga Maisha yako katika mchezo wa redio ” **WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- huu ukiwa ni mchezo unaomulikia vita vya familia moja dhidi ya Malaria**”...Wiki iliyopita Familia ya Masika ilipata mgeni kwa jina zawadi na kupitia kwa mwalimu mkuu, Karembo alijifunza kuhusu kinga ya malaria kwa kutumia neti iliyotibiwa kwa dawa ya kuua wadudu.... je wataitumia neti hiyo kwa muda gani na kuna athari gani inayotathminiwa kuwakumba wale wasiolala chini ya chandarua cha neti? Jiunge nasi upate kusikia haya na mengineyo katika kujifunza juu ya ” **ISHARA NA MATIBABU”**

**MUSIC INTERLUDE**

**<u>SCENE ONE: MORNING AT MASIKA’S HOME</u>**

**A-SFX: COCK CROWS, BIRDS SINGING**

| | | |
|---|---|---|
| **1.** | **BETTINA:** | (**CALLS OUT**)<br>Karembo! Kumepambazuka sasa.. ni saa kumi na moja... nahitaji maji nimuogeshe zawadi,kisha umtayarishie babako kiamsha kinywa na ujitayarishe kwenda shule... karembo! |
| **2.** | **KAREMBO:** | (**WAKING UP)**<br>Mmmh..Ah! Mama... sihisi vizuri leo... |
| **3.** | **BETTINA:** | Naelewa hakuna apendaye kuamka mapema jimbi la kwanza lakini ni sharti uamke unisaidie... |
| **4.** | **KAREMBO:** | Hasha! Sijakana kukusaidia mama.. (**CRIES IN** |

**PAIN)**…
lakini nasikia mwili wote uko uchungu,sio kichwa.. mgongo... viungo... kila pahala..

**5. BETTINA:** Usitake kunizaa upya! Usinidanganye! Hata mimi niliupitia huo umri wako ,hebu ondoka ukanichotee maji,sitaki kuchelewa kumpeleka zawadi kupata chanjo yake ya kwanza kliniki.

**6. KAREMBO:** **(unhappy)**
Mama sikudanganyi... nishike unihisi nilivyo na joto mwilini basi... sadiki nisemayo...

**7. BETTINA:** Sawa... nakuamini**....(SHOUTS)**
haya nenda kanichotee maji!..

**8. B-SFX: ZAWADI/BABY STARTS TO CRY**

**9. BETTINA:** Waona sasa umemuamsha mtoto? Basi bas... totooooo... ooooh... baaas.... bachi nchocho wangu...

**10. KAREMBO:** Samahani mama basi nitaenda...... mama je ulionaje kulala ndani ya neti?umefurahia?

**11. BETTINA:** Tena sana! Sijawahi kupata usingizi mzito kwa muda mrefu kama leo... haya, kazana mwanangu kabla babako haja amka akakuta hakuna cha maana tulichotenda... haya chapuka!

**12. NARRATOR:** Ilitamkwa jadi na jadi kuwa kinga ni bora kuliko tiba! Na kutambuwa mapema dalili za malaria ni muhimu ili kuzuia maradhi haya kuwa janga! Lakini mapuuza au kutojulikana kwa dalili hizi na wengi ni jambo la kawaida. Betina , mamake Karembo ni mmoja wa wasiojali dalili hizi.alimlazimu Karembo kufanya kazi za nyumbani na kwenda shuleni ambapo mambo yanakwenda mrama, lakini kabla ya hapo kwanza tumpe jicho jirani yao, mama david..

**<u>SCENE TWO: MORNING AT MAMA DAVID'S HOUSE</u>**

**13. C-SFX: TEA BEING POURED IN CUP**

**14. MAMA DAVID:** (**CALLS OUT)**
David! chai tayari mwanangu... harakisha au itapoa...

**15. DAVID:** **(GRUMBLING)** Mama mimi si mtoto! Kila siku hukueleza kuwa nimetimu umri wa kujiandalia chai mimi mwenyewe..

**16. MAMA DAVID:** Siamini usemayo kwani kama umekuwa kweli, mbona chumba chako ni kama zizi la nguruwe? Uchafu umetapakaa kama jalala?

**17. DAVID:** Sawa nitasafisha,una jengine?

**18. MAMA DAVID:** Ndiyo.Unaona huu moshi wa dawa ya mbu.. sio mwema kwa afya yako.. kifua chako kitadhurika... acha kuchoma dawa ya mbu... si moshi, harufu au hata jivu lake halinipendezi kamwe!

**19. DAVID:** Basi uko kama huyo mbu mwenyewe!! . **(LAUGHS)**

**20. MAMA DAVID:** Wewe huna adabu unaniita mimi mbu? (**SHOCKED)**
Tangu lini nikiwa usubi? Waniita mbu?

**21. DAVID:** La! La mama... nilimaanisha uninunulie neti ya kujikinga na mbu.

**22. MAMA DAVID:** Usinifanye kujuta kwanini nilikuzaa... ningelifurahi sana kama ungelikuwa kama Karembo. Mbona usiwe kama yeye? Au usijaaribu kumuiga miondoko yake?

**23. DAVID:** Kusema kweli nampenda sana Karembo...aah nikimaanisha .. napendezwa na Karembo..

**24. MAMA DAVID:** Laitani babako angelikuwa hai akakusikia ukitamka huo upuuzi wako... angeliku.....(**STARTS TO CRY)**

**25. DAVID:** Samahani... mama nisamehe sitorudia... nitabadili tabia zangu.. nitanadhifisha chumba changu na nitakoma kuchoma hiyo dawa ya mbu... lakini

nahofia kupata ugonjwa huu wa malaria...(**PAUSES)** na kufariki kama baba alivyofariki

**26. MAMA DAVID:** Marehemu babako hakufariki kwa ajili ya malaria... ali......**(CRIES MORE)**

**27. DAVID:** Mama, najuwa huziamini hizi dawa za siku hizi zinazouzwa madukani.. lakini ni lazima usadiki kuwa baba aliaga dunia kwa sababu aliuguwa sana kabla ya kupata matibabu... labda tungelikuwa naye leo kama angelitibiwa hospitali kwa wakati unaofaa..na mama, dawa za mbu si hatari kwa wanadamu kwa sababu zimetengenezwa na maua ya pyrethrum ambayo...

**28. MAMA DAVID:** **(CHANGES TOPIC)**
Maliza kunywa chai , uende shule...

**29. NARRATOR:** Vita dhidi ya malaria vinarudishwa nyuma na mengi yakiwemo itikadi na hekaya kuuhusu ugonjwa huo. Mamake david aliamini kuwa malaria ni pepo mchafu na lazima atolewe na mganga au mchawi.Shuleni, wakati ulivyozidi kwenda nayo homa ya Karembo ilizidi kupanda. Kwa Sadfa Masika, babake,Karembo aliamka na kukuta hamna mtu nyumbani, akachukuwa neti iliyotibiwa kukingia mbu na kwenda nayo baharini kuvulia samaki... lakini kwanza tujiunge naye

Karembo akiwa afisini kwa mwalimu mkuu.

**SCENE THREE: HEADTEACHER'S OFFICE**

**30. KAREMBO:** (**SHIVERING IN BETWEEN LINES)** Mwalimu mkuu... nimekuja kuomba ruhusa ya kurudi nyumbani,sijiskii vyema leo..

**31. HEADTEACHER:** Nilijuwa unaumwa... tazama unavyotetema kama jani la mti katika kipupwe.. nitakuandikia idhini uende nyumbani lakini lazima iwekwe sahihi na daktari kama ishara ya kuwa umetibiwa.

**32. KAREMBO:** Nashukuru.. mwalimu.. naweza kukuuliza swali?

**33. HEADTEACHER:** Wewe huchoki kuuliza maswali? Haya uliza.

**34. KAREMBO:** Mwalimu... unafikiria mimi nina malaria?

**35. HEADTEACHER:** Hilo mwanangu ni swali ambalo daktari pekee ndio anaweza kukujibu... mimi siwezi.. unajuwa dalili za malaria huambatana na dalili za maradhi mengi mengine... sio rahisi kuutambuwa kwa kutazama sharti upate vipimo.. usiwe na hofu.. malaria hutibika inapopata matibabu mazuri na wakati unaofaa.. sawa?

**36. KAREMBO:** Sawa mwalimu mkuu... asante.

**37. D-SFX: DOOR CLOSES**

**NARRATOR: Mchezo unapozidi kupamba moto K**arembo alikwenda nyumbani huku akikosa nusu ya siku ya masomo yake... takwimu zinaonyesha kuwa watoto wengi hupoteza asilimia 60 ya wakati wao wa masomo kutokana na malaria, karembo alifika nyumbani akiwa mchovu, akihisi kizunguzungu na homa kali lakini alipofika alipigwa na butwaa.

**SCENE FOUR: AT MASIKA'S HOME…KAREMBO ALONE AT HOME**

**38. MUSIC INTERLUDE**

**39. KAREMBO:** (**FAINT WEAK VOICE)** Mama! hodi, inaonekana hakuna mtu hapa nyumbani,nahisi ni kama kuna mtu anatwanga mahindi kichwani mwangu...acha nilale ndani ya neti maana mama na zawadi hawako....

**40. E-SFX: DOOR OPENS.**

**41. KAREMBO:** Ha!(**SURPRISED AT NOT SEEING THE NET)**kwani naota? neti iko wapi? Nilifikiri mama alisema kuwa alilala vyema.... **(COMES TO REALIZATION)**la! Hapana! Baba! Lazima baba ameichukuwa...

**42. F-SFX: DOOR OPENS, MASIKA HEARD WHISTLING**

**43. MASIKA:** **ENTERS HAPPY, WHISTLING...**

**44. KAREMBO:** Habari ya mchana baba?

**45. MASIKA:** (**CAUGHT BY SURPRISE)**
Ala! karembo? Unafanya nini hapa? Si watakiwa kuwa shule!

**46. KAREMBO:** Ndio... lakini sihisi vyema.. naumwa... nilimweleza mama asubuhi lakini hakuniamini... nilipofika shule nilizidiwa ndiposa ikanilazimu kuomba ruhusa... baba, iko wapi neti ya kujikingia mbu? Siioni ikinin'ginia kitandani?

**47. MASIKA:** **(IGNORES QUESTION)**
unashida gani? Unaumwa na nini?

**48. KAREMBO:** Nahisi ovyo! Viungo vyote vyaniuma! Kichwa pia.. nilitetema sana nikiwa darasani... singeweza kuweka makini masomoni... lakini baba... neti iko wapi?

**49. MASIKA:** Aah inaonekana una homa... hebu jitulize kidogo, nitakununulia tembe za klorokuini.. na nyengine za maumivu...ikifika kesho utahisi afueni.

**50. KAREMBO:** Kumradhi baba..nakuuliza kuhusu neti.. iwapi?

**51. MASIKA:** **:** Neti? Aah ile neti nimeihitaji siku nyingi ..... wajua nimeitupa baharini tu na ikashika samaki wengi sana! Sasa tunakitoweo cha siku mbili! Si baraka hizo?

**52. KAREMBO:** Lakini baba.. hiyo neti ililetwa kwa azimio la kumkinga mtoto wetu zawadi dhidi ya malaria kutokana na michomo ya mbu.. uliichukuwaje kwenda kuvulia samaki?

**53. MASIKA:** Usinibughudhi! (**ANNOYED)** sasa ningefanyaje? Tumkinge zawadi kutokana na usubi halafu tumwangalie akifa kwa njaa? Ungali mtoto sana hujui hujuma za ulezi...sasa nakuamuru ulale na sitaki kukusikia ukinifunza jinsi ya kuilea familia yangu... nakuletea dawa sasa hivi...

**NARRATOR:** Je, Masika alifanya jambo la busara kuitumia neti kuvulia samaki kwa azimio la kuilisha familia yake? Usinijibu kwa sasa.. lakini jambo lakusikitisha ni kuwa alimuacha kijana wake bila kinga yeyote dhidi ya mbu anayesababisha malaria..” wageni wasioalikwa” kama anavyowaita Karembo mwenyewe...jioni inapobisha, Bettina alirudi lakini hata hakugunduwa kuwa neti hiyo haikuwepo nyumbani kwa sababu Karembo alikuwa mgonjwa kitandani, baadaye akaamua kumtembelea mama david kwa ushauri.

**<u>AT MAMA DAVIDS HOUSE</u>**

**54. MAMA DAVID:** Hebu punguza hamaki.. tulia betina.. nieleze karembo hali yake iko vipi haswa?

**55. BETTINA:** **(PANICKY VOICE)**
Hajawahipo kudhoofika hapo awali namna hii, anatetema chini ya blanketi na mwili wake una

joto jingi...mdomo umefanya kibimbi,hataki kula.sijui nitafanyaje.

**56. MAMA DAVID:** Basi tulia... atapona tu,muwekee tambara la maji kipajini mwake na umfunike na blanketi nyengine zaidi.. kadri anavyotokwa na jasho ndio malaria inavyomtoka mwilini... akiamka kesho atakuwa buheri wa afya kama mtoto mchanga...

**57. BETTINA:** Na dawa je? Mumewangu alikuwa tayari ashampa klorokuini.. je tumpe nyengine kuondoa hiyo homa?

**58. MAMA DAVID:** Abadan! Usimpe chochote ila chakula tu.. mwili wake unahitaji nguvu kupambana na hiyo malaria... kesho nitawapitia kumwona anaendeleaje..

**59. BETTINA:** Nimeshukuru sana kwa ushauri wako.. nilikuwa sijui la kufanya.. usiku mwema.

**60. MAMA DAVID:** Karibuni... hata nanyi muwe na usiku mwema, mwambie Masika nahitaji samaki aniletee.

**61. G-SFX: DOOR OPENS, CLOSES**

**OUTRO/NARRATOR:**

Alipoelezwa haya Betina alikurupuka mbio hadi kwake aweze kufanya alivyoshauriwa na mama david kuhusu karembo.....je, itafanya kazi? Itamponesha karembo? Na je, zawadi naye atakumbwa na yapi asipolala

chini ya neti usiku huo? Je, elimu ya karembo itachukuwa mkondo upi atakapokuwa ugonjwa umemzidia? Kwa haya na mengineo jiunge nasi katika kipindi kijacho cha nne katika mchezo **"WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA KATIKA VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA".**

Tafadhali tuma maoni yako au hoja zako au unapotaka kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea tovuti www.dw-world.de/lbe

Hadi wakati mwengine.kwaheri .